Inavyodaiwa na wanaochanganya Biblia

na

Ellis Forsman

Inavyodaiwa na wanaochanganya Biblia

na

Ellis Forsman

Oktoba 8, 2011

Inavyodaiwa na wanaochanganya Biblia

1 Tim. 6:20-21

1 Tim.6: 20-21, *"Ee Timotheo, ilinde hiyo amana; ujiepushe na maneno yasiyo ya dini, yasiyo na maana, na mashindano ya elimu iitwayo elimu kwa uongo; ambayo wengine wakiikiri hiyo wameikosa Imani. Neema na iwe pamoja nanyi.*

Biblia ni neno la Mungu. Imejithibitisha yenyewe kuwa ni kweli.

Unabii wa Agano la kale kuhusu Masihi ili timizwa karne nyingi baadaye.

Wakati wa zamani Mungu aliongea na watu wake kupitia manabii. Baada ya kusulubiwa kwake, Kristo alituma Roho Mtakatifu kuwaongoza mitume katika kuanzisha neno lake.

- Yoh.16:13, "*Lakini yeye atakapokuja, huyo Roh wa kweli atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mweyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari zake."*
- 2 Petr1:21, "*Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya wanadamu, bali wanadamu walinena, yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu."*
- 1 Wathes. 2:13, "*Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma kwa kuwa, mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadanu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo ilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini."*

Biblia imevuviwa.

- Zaburi 19:7, "*Sheria ya BWANA ni kamilifu huiburudisha nafsi, Ushuhuda wa BWANA ni amini, humtia mjinga hekima.*
- Zaburi 119:89, *"Ee BWANA neno lako la simama imara mbinguni hata milele."*
- Yohana 10:35, "Ikiwa aliwaita miungu iliyojiliwa na neno la Mungu; na maandiko hayawezi kutanguka."
- Math. 5:17-18, "*Kwa maana amin, nawambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie."*

Kuna waongo wengi katika ulimwengu

Miongo mingi iliyopita kume kuwa na pingamizi nyingi kwamba Biblia ni neno la Mungu, au kwamba hata wazo la Mungu yupo.

Mitume walipambana na tatizo hili,na kuthibitisha vitu walivyosema vilikuwa ni kweli kupitia Miuji waliyofanya.

Waeb. 2:3-4, *"Sisi je! Tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu wa namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kasha ukathibitishwa kwetu na waliosikia; Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyo penda mwenyewe."*

Nilipokuwa takribani miaka 17 katika shule ya secondary (upili), mwenzangu alinishangaa nilipotaja baadhi ya mistari ya Biblia na akaniambia hakutaka kusoma Biblia, kwa ilikuwa na uchanganyifu mwingi. Nikamwuliza anipe mfano wa kuchanganyikiwa huko. Atamwuliza baba yake ambaye alikuwa hamwamini Mungu.

Baada ya hapo, alionekana kama ananikwepa. Baadaye tulipokutana na nikaendelea kumkandamiza katika swala hili, akasema, "sina muda wa kwenda na kutafuta kitu ambacho si cha kweli!" hakuniambia kile alichodai kuwa ataniambia.

Mifano ya kujichanganya imeelezwa

Je Mungu ni wa vita au amani:

- Rumi. 15:33, *"Na Mungu wa amani awe nanyi nyote. Amen."*
- Kuto. 15:3, "*BWANA ni mtu wa vita, BWANA ndilo jina lake."*

Mungu ni mtu wa vita kwa maadui zake na Mungu wa amani kwa marafiki zake. Anawaadhibu wasio na mungu na anawazadi wenye haki.

Rumi. 11:22, *"Tazama, basi wema na ukali wa Mungu; kwa wale walioanguka, ukali, bali kwako wewe wema wa Mungu, ukikaa katika wema huo, kama sivyo wewe nawe atakatiliwa mbali."*

Je sheria ya Mungu ni kamili kwa chochote?

- Yakobo 1:25, "*Lakini aliyeitazama sheria kamilifu ilio ya uhuru na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake."*
- Waeb. 7:19, *"(kwa maana ile sheria haikukamilisha neno); na pamoja na hayo kuliingizwa matumaini yaliyo mazuri, ambayo kwa hayo twamkaribia Mungu."*

Kifungu cha kwanza kinazungumzia sheria ya Agano Jipya, kifungu cha mwisho kinazungumzia Agano la Kale ambayo haikukamilisha kitu.

Ni watu wangapi vipofu waliomkaribia Yesu?

- Math. 20:30, "*Na tazama vipofu wawali wameketi kando ya njia, nao waliposikia ya kwamba Yesu anapita, walipaza sauti, wakisema, Uturehemu Bwana Mwana wa Daudi."*
- Luka 18: 35-38, "*Ikawa alipokaribia Yeriko, mtu mmoja kipofu alikuwa ameketi kando ya njia, akiomba sadaka, na alipowasikia makutano wakipita, aliuliza, kuna nini? Wakamwambia Yesu wa Nazareti anapita. Akapiga kelele akisema, Yesu Mwana wa Daudi, unirehemu."*

Jibu liko katika misitari inayoendelea katika Mathayo, *"Na walipoondoka Yeriko,watu wengi wakamfuata."* (Math. 20:29). Luka aliandika tukio wakati kipofu mmoja akiomba wakati Yesu alipokuwa anaingia Yeriko. Mathayo akaandika tukio la vipofu wawili wakiomba wakati Yesu alipoingia Yeriko. Mkanganyiko uko wapi?

Je Yesu aliruka kutoka katika kifo?

- Yoh. 12:27, *"Sasa roho yangu imefadhaika nisemeje? Baba uniokoe katika saa hii? Lakini ni kwa ajili ya hayo nilivyoifikia saa hii."*
- Wafil. 2:8, "*Tena alipoonekana ana umbo kama la mwana damu alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba."*

Kama mwanadamu Kristo alitoka katika wafu. Hakusitaili kufa. Kama Mwana wa Mungu alikuja kufanya mapenzi ya Baba yake. Hii inajumlisha kifo chake. Aliomba, *"sio mapenzi yangu bali mapenzi yako yatimizwe."* Kristo alitimiza wajibu wake hatakama ili mugharimu mateso. Hili linapaswa kuwa tukio la kutamanisha. Hataivyo Yesu hakutaka kufa, aliteseka msalabani kwa ajili yetu.

Ni wanawake wangapi waliokuja katika kaburi la Yesu?

- Yoh. 20:1, *"Hata siku ya kwanza Mariam Magdalene alikwenda kaburini alfajiri, kungali giza bado, akaliona lile jiwe limeondolewa kaburini*
- Math. 28:1, "*Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariam Magdalene, na Mariam Yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi."*

Yohana anasema kuwa Mariam Magdalena alikwenda asubuhi katika kaburi, haisemi kwamba alikuja peke yake. Mathayo naye anarudia kitu kile kile na kuongeza kuwa Mariam mwengine naye alikuja.

Kwa mfano, naweza nikakwambia kuwa Terry alikwenda kwa sababu alikwenda Oklahoma kuendesha semina; na naweza kumwambia mtu tofauti kwamba Terry na Richard wamekwenda Oklahoma kuendesha mkutano. Maneno haya yote yanaweza kuwa ya kweli.

Je Mungu anakubali wizi?

- Kutoka 3:21-22, *"Nami nitawapa watu hao kufdhiliwa mbele ya Wamisri, hataitakuwa hapo mtakapokwenda zenu, hamta kwenda kitupu. Lakini kila mwana mke ataomba kwa jirani; na kwa huyo akaye naye nyumbani, vyombo vya fedha na vyombo vya dhahabu, na mavazi nanyi mtawavika wana wenu na binti zenu, nanyi mtawateka nyara Wamisri."*
- Kutoka 12:33-36, "*Twaeni kondoo zenu na ng'ombe zenu kama mlivyosema, enendeni zenu mkanibariki mimi pia, Wamisri nao wakawahimiza watu, kuwatoa katika nchi kwa haraka, maana walisema Tumekwisha kufa sote. Watu wakauchukua unga wa mikate yao kabla haijatiwa chachu na vyombo vyao vya kukandia wakavitia ndani ya nguo zao mabegani. Wana wa Israeli wakafanya kama neno lile la Musa; wakataka kwa Wamisri vyombo vya fedha, na vyombo, vya dhahabu, na mavazi. BWANA akawajalia kupendelewa na Wamisri hatawakawapa kila walichokitaka. Nao wakawateka Wamisri nyara."*
- Walawi. 19:13, "*Usimdhulumu jirani yako,wala kumnyang'anya mali yake, ijara yake aliyeajiriwa isikae kwako usiku kucha hata asubuhi."*
- Kutoka 20:15, *"Usiibe"*

Kwa miaka 250 Waisraeli walitumika kama watumwa katika nchi ya Misri. Wali jaza vitu vingi katika serekali ya Misri. Ulipofika muda wa kuondoka, waliomba dhahabu, fedha, na mabaki ya wale walioiba, wakateswa na kutumikishwa kwa karne nyingi. Neno lililo tafsiriwa "azima" kwa hakika haimaanishi "kuazima" lakini pia inaonyesha "kuuliza" au "kudai". Ilikuwa ni swala la haki, sio wizi.

Lazima watu wawadharau wazazi wao?

- Luka 14:26, "*Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake, naam, na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu."*
- Waef. 6:2, *"Waheshimu baba yako na mama yako, amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi."*
- Waef. 5:25, "*Enyi waume wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake."*

Katika Luka 14:26 neno "Chukia" kirahisi inamaanisha kutokupenda. Mtu anayempenda baba yake au mama yake, au mwanamke, au wato zaidi ya Bwana, hawezi kuwa mwanafunzi wa Bwana. Tunapaswa kuwaheshimu wanajamii zetu, lakini tusiwapende sana kuliko Bwana. Njia nyingine ya kusema hili ni kwamba, tunapaswa kumpenda Mungu kuliko waume zetu,au wake zetu, watoto wa kiume na wa kike, hata uhai wetu.

Je nilazima watu watii sheria za nchi?

- Waru. 13:1, *"Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu, kwa maana hakuna mamlaka isiyitoka kwa Mungu, na ile iliyopo umewekwa na Mungu."*
- 1 Petr. 2:13-14, "*Tiini kila kiamuriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana ikiwa ni mfalme mwenye cheo kikubwa; ikiwa ni wakubwa, kama wanotumwa naye ili kuwalipiza kisasi watenda mabaya na kuwasifu na kuwasifu watenda mema."*
- Kutoka 1:17,*"Lakini wale wazalisha walikuwa wakimcha Mungu, wasifanye kama walivyoamriwa na huyo mfalme wa Misri, lakini wakawahifadhi hai wale wanaume."*

Biblia inafundisha kwamba lazima tueshimu sheria za nchi. Tunapaswa kuziheshimu katika kila kitu ambacho ni haki. Kama serikali itatulazimisha kufanya kitu ambacho siyo sahihi, tunatakiwa kukataa kufanya hivyo, sawa na wana wake wa kati walivyo kataa kutii

amri ya mfalme, kwa sababu walimwogopa Mungu kuliko mwandamu. Wakati sheria ya mwanadamu inapingana na sheria ya Mungu, ni lazima tumtii Mungu kuliko mwanadamu.

Mitume walizuiwa na sheria kuhubiri, lakini walihubiri hata ivyo. Walimuheshimu Mungu kuliko mwanadamu kulipokuwa na tatizo.

Wakati Mfalme Daria alipozuia maombi, Danieli aliomba mara tatu kwa siku kama kawaida yake.

Je ubatizo umeamriwa?

- Math. 28: 19-20,*"Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari."*
- 1 Wakor. 1:17, *"Maana Kristo hakunituma ili nibatize; bali niihubiri Habari Njema, wala si kwa hekima ya maneno, msalaba wa Kristo usije ukabadilika."*

Yesu Kristo aliamuru ubatizo. Aliwaamuru wanafunzi wake kufundisha na kubatiza watu wote katika ulimwengu anayependa kuwa Mkristo. Kauli ya Paulo katika 1 Wakoritho lazima izingatiwe katika mazingira yake. Alikuwa na furaha kwa sababu hakubatiza kamwe Wakoritho aliyo kuwa nao, ili mtu asije akasema kuwa alibatiza kwa jina lake mwenyewe. Wengine walio safari na Paulo walifanya ubatizo mwingi. Kazi ya Paulo ilikuwa ni kuhubiri injili, hata ivyo alibatiza baadhi yeye mwenyewe.

1 Wakor. 1: 11-16, *"Kwa maana ndugu zangu nimearifiwa habari zenu, na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu. Basi, maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, mimi ni Paulo, na mimi ni wa Kefa, na mimi ni Apolo, na mimi ni wa Kristo. Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? Au je mlibatizwa kwa jina la Paulo. Nashukuru kwa sababu sikubatiza mtu kwenu ila Krispo na Gayo; mtu asije akasema kwamba mlibatizwa kwa jina langu. Tena naliwabatiza watu wa nyumbani mwa Stefana, zaidi ya hao sijui kama nalimbatiza mtu yeyote mwingine."*

Je kifo bado kipo?

- 2 Tim. 1:10,*"na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake mwokozi wetu Kristo Yesu; aliye batili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika kwa ile injili."*
- Waeb. 9: 27, *"Na kama vile wayu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu."*

Yesu Kristo alianzisha kifo kama cha jumla. Ametoa uchungu wake na maumivu ilikwamba isiwe inatumaliza. Kristo anaufungu wa kaburi. Ikifuatiwa na kufufuka kwa Kristo, mitume walichukulia kama kifo cha kimwili lakini ni mlango wa kupitia kwenda katika maisha mengine na Mkuu wao. Hawakuogopa kifo.

Je Kristo anahukumu?

- 2 Wakor. 5:10, *"Kwa maaana imetupasa sisi sote kudhiirika mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya."*
- Yoh. 8:15, *"Ninyi mwahukumu kwa kufuata mambo ya mwili; mimi simhukumu mtu."*

Katika kuja kwake mara ya kwanza, Kristo hakuonekana mwenyewe kama mhukumu, ila kama Mkombozi wa wanadamu. Alikuja kuokoa. Kuja kwake mara ya pili atawalipiza kisasi *"kwa wale wasiyomjua Mungu, na kwamba hawakutii injili ya Bwana wetu Yesu Kristo:* (2 Wathes. 1:8).

Je dunia itaharibiwa?

- Zaburi 78:69, *"Akajenga patakatifu pake kama vilele, kama dunia aliyoiweka imara milele."*
- Mhubiri 1: 4, *"Kizazi huenda, kizazi huja, nayo dunia hudumu daima."*
- Math. 24:35, *"Mbingu na nchi zitapita lakini maneno yangu hayatapita kamwe."*
- 2 Petr. 3:10, *"Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea."*

Neno la Kiyunani “olam” imetolewa “milele” haina mwisho, kiwango cha muda usiojulikana- mud mrefu, mwisho tuliyofichwa. Dunia haitakaa milele.

Kristo anatujengea mji mpya.

Yahana 14: 2-3, *“Nyumbani mwa Baba yangu mna makao makao mengi, kama sivyo ningaliwaambia, maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi, nanyi mwepo.”*

Hitimisho

Kuna vitu vingi katika Biblia ambavyo watu wabaya watabadilisha wakitafuta mkanganyiko ili kwamba wasiipe sifa Biblia. Vitu ambavyo wanaweza kutoka navyo vinashangaza mno. Biblia ni kweli. Imejithibitisha yenyewe kuwa hivyo.

Na kama Biblia ni kweli, basi madhara inayozungumzia pia ni kweli.

Mbingu na jehanamu ni hakika, sawa sawa na hukumu kuu. Jiandae kwa hilo tukio kuu leo, wakati kukiwa na muda. Mtu anaweza kuokolewa vipi? Mtu lazima awe mkristo.

Yafuatayo ni hatua mhimu inayofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, *“Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.”* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana wa jirani miaka sawa na yangu akaniambia hamtambui Mungu. Kwa sababu nilikuwa nimesha batizwa, nilichukuwa nafasi niongee naye kuhusu maandiko. Akaniambia kuwa kuishi maisha ya Ukristo ilikuwa nzuri, lakini alikuwa haamini kuwa kuna Mungu. Lakini katika kuwa upande salama, labda angekwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele ya Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani, na kuishi maisha mazuri Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na si kuzimu (kama kuna kuzimu). Nikamwambia, “haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima umuamini kwa moyo wako wote, lasivyo, huwezi kumpendeza.”

- **Toba.** Matend. 2:38, *“Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”* Matend. 11: 18, “...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao *toba liletalo uzima,”*

wakati ulipokuwa inalala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na ukafikiria wewe mwenyewe, “kuna kitu ndani mwangu!” sasa unachukuwa simu ya mkononi, na kwa haraka uwezavyo, unawaita polisi, kuna mwizi katika nyumba yangu, na unawapa namba ya nyumba yako. Kidogo, unawasikia wamefika na kumshika mwizi. Anapiga kelele, “samahani!” Anaomba msamaha juu ya nini? Anaomba msamaha kwa sababu ameshikwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi huyu angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadili maisha yake ili kwamba asiibe tena. Hiyo ni toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Warumi 10:9-10, *“Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.”* Tuna kiri nini? Kwamba tunaamini kuwa Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni “**KATIKA**” haki, maisha au wokovu. “Katika” inamaanisha kuelekea katika kitu Fulani; siyo kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo**. Ni katika ubatizo ndipo haki, maisha, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa kutimiza haki yote, “*Lakini, Yohana alitaka kumzuia, akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa; kwa sababu ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake. Na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.”* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi kuifanya. Unaona jinsi Mungu alivyopendezwa Yesu alipo batizwa? Yesu pia alisema *“imekuwa “**sisi”** kutimiza haki yote.”* Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake, siyo kwa sababu ni ya haki yetu.

  Hakika, tusipo batizwa, bado tupo katika dhambi zetu. *“Basi, Petro akawaambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”* (Matnd.2:38). Petro, ulisema sababu ya

ubatizo ni nini? *"kwa ajili ya ondoleo la dhambi".* Kwa nini mtu anataka kuacha hatua inayo ondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kuwa ili tuufikie wovu ni lazima tubatizwe. "*Akawaambia, nendeni ulimwengu kote, mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka; asiye amini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambi Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu hicho icho, *"Sasa unakawilia nini? Simama, na ubatizwe uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Mtend. 22:16).

Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* Utuwetu wa kale lazima ufe, "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu, tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake. Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."* (Warumi 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa njia ya ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza" maandiko hapo juu yanasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki maiti makaburini na kuchukuwa udongo mdogo na kuweka juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujawa Kristo, kwa nini usianze leo?